



**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU
TANZANIA**



TAARIFA KWA UMMA

**TAKWA LA LAZIMA LA UPIMAJI WA MABAKI YA VIUATILIFU
(PESTICIDE RESIDUES) NA SUMU KUVU (AFLATOXIN) KWA UFUTA
UNAOKWENDA JAPAN**

26 February 2026, ARUSHA

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania inapenda kuwataarifu Wakulima, Wanunuzi, Wasafirishaji na Wadau wote wa zao la Ufuta kuwa, kufuatia matakwa ya soko la Japan, kuanzia tarehe ya tangazo hili:-

- 1. Upimaji wa mabaki ya Viuatilifu na Sumu Kuvu ni wa Lazima**
Shehena zote za Ufuta zinazokusudiwa kusafirishwa kwenda Japan lazima zipimwe:-
 - i) Mabaki ya Viuatilifu (Pesticide Residues); na
 - ii) Sumu kuvu (Aflatoxin)

Upimaji utafanyika katika maabara za TPHPA au maabara zitakazotambuliwa rasmi na Mamlaka.

- 2. Hakuna Cheti Bila Majibu ya Maabara**
Mteja hatapatiwa Cheti cha Usafi wa Mazao (Phytosanitary Certificate) bila kuwasilisha na kuthibitisha majibu ya maabara yanayoonesha kuwa:-
 - i) Viwango vya mabaki ya Viuatilifu vinazingatia viwango vinavyokubalika katika soko la Japan; na
 - ii) Viwango vya Aflatoxin vipo ndani ya mipaka inayokubalika Kimataifa na soko husika.

- 3. Inahusu Hata UfutaAmbao Haujasafirishwa**
Tangazo hili linahusu pia Ufuta uliopo maghalani au ambao haujasafirishwa, kabla ya kuomba cheti cha usafirishaji kwenda Japan, ni lazima upimwe na kuthibitishwa kukidhi viwango vya mabaki ya Viuatilifu na Sumu kuvu vinavyotakiwa.

4. Uwajibikaji wa Wadau

Wadau wote wanatakiwa kuhakikisha:-

- i) Matumizi sahihi ya Viuatilifu vilivyosajiliwa.
- ii) Kuzingatia muda wa mwisho wa matumizi kabla ya kuvuna (Pre-Harvest Interval-PHI).
- iii) Uvunaji, ukaushaji na uhifadhi bora wa Ufutailiaji kuzuia maambukizi ya fangasi yanayosababisha Sumu kuvu.
- iv) Kuhifadhi kumbukumbu sahihi za matumizi ya pembejeo na taarifa za uzalishaji kwa ajili ya ufuatiliaji (traceability).

Hatua hizi zinalenga kulinda masoko ya Kimataifa, hadhi ya Ufuta wa Tanzania, usalama wa walaji na kuzuia kurejeshwa kwa shehena (rejection) katika soko la Japan.

Tunatoa wito kwa Wadau wote kushirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa maelekezo haya.

Kwa mawasiliano zaidi, **tafadhali tuma barua pepe kupitia: dg@tphpa.go.tz au wasiliana nasi kwa simu:+255782146161.**

Imetolewa na,



Prof. Joseph O. Ndunguru
MKURUGENZI MKUU